JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA NZEGA

SHULE YA SEKONDARI PUGE

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI PUGE



CamScanner

*JAMHURI YA* MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI

HALMASHAURI YA WILAYA YA NZEGA

Namba za simu: a

Makamu mkuu wa shule: 0783123777

SHULE YA SEKONDARI PUGE

S.LP 82

NDALA – NZEGA.

*TAREHE*:……………………………………….

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi……………………………………

………………………………………………………………………

S.L.P………………………………

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI PUGE HALMASHAURI YA WILAYA YA NZEGA MKOA WA TABORA MWAKA……………………..**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule hii mwaka………………… na atasoma tahasusi ya PCM, EGM, EBuCA.

   Shule ya sekondari Puge ipo umbali wa kilometa 59 kutoka Nzega mjini na kilometa 56 kutoka Tabora mjini. Usafiri wa basi kutoka mjini unapatikana katika kituo cha mabasi Nzega mjini na Tabora mjini, nauli ni shilingi 4,000/= kwa basi.

   Muhula wa Masomo unaanza tarehe……………..hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni ……………………

   tarehe …………………… Mwisho wa kuripoti tarehe……………

## 2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:

### 2.1. Sare za shule

**a. Wavulana:**

(i) Shati *mbili* (2) nyeupe zenye mikono mirefu, suruali mbili (2) bluu **bahari** zenye marinda mawili kila **upande.(ZISIZOBANA, ISIWE Model")na** tai mbili (2) bluu bahari. **Zitakaguliwa.**

(ii) Soksi nyeusi ndefu pea mbili(2)

(iii) Aje amevaa suruali ya Light blue zenye malinda mawili kila upande na shati la shule (ambalo halibai).

(iv) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.

(v) Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali,

(vi) Sweta la rangi ya kijivu mikono mifupi (Kizibao)

(vii) Nguo za kushindia (shamba dress) Tshirt (02) rangi ya kijivu na suruali (02) dark blue.

(viii) Tai mbili (02) rangi za light blue

(ix) Sare ya michezo Track suit rangi ya dark blue pair 1, Raba jozi moja ya kufunga na kamba.

b. **Wasichana**

(i) Sketi mbili rangi ya light blue (mshono wa linda box) (iwe ndefu mpaka kwenye kifundo cha mguu).

(ii) Shati mbili nyeupe mikono mirefu (zitakaguliwa).

(iii) Viatu pea mbili vyeusi, kisigino kifupi, vya kufunga na kamba

(iv) Soksi nyeupe ndefu (pea mbili)

(v) Sweta rangi ya kijivu mikono mifupi (Kizibao)

(vi) Tai mbili (02) rangi za light blue

(vii) Hijabu ndefu rangi nyeupe mbiliisiwe **mtandio**

(viii) Nguo za kushindia (shamba dress) sketi rangi ya dark blue (mshono linda box) ndefu hadi kwenye kisigino.

(ix) Tshirt rangi ya kijivu yenye kola (aje amevaa pamoja na sketi ya dark blue)



CamScanner

(x) Sare ya michezo Track suit rangi ya kijivu pair I, Raba jozi moja ya kufunga na kamba.

NB: mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo za ziada tofauti na maelekezo **haya**.

**2.2. Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:**

(i) Trunker

(ii) Madaftari 'Counter book' Quire 4' ya kutosha (10 au Zaidi)

(iii) Ream paper (A4) mbili (2) kwa **mwaka.(double A/Bright white multi- purpose office paper)**

(iv) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika

(v) Dissecting Kit, pamoja na Scientific Calculator

(vi) Godoro lenye ukubwa wa futi *2.5* upana na urefu futi 6

(vii) Mashuka Jozi 2 rangi ya pink, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 futi 3% kwa6

(viii) Nguo za ndani za kutosha mahitaji ya mwanafunzi binafsi

(ix) Vyombo vya chakula: Sahani ya bati I, Bakuli ya bati 1, kijiko 1, kikombe cha bati 1, Ndoo za plastiki 2 zenye mifuniko.

(x) Kwanja 1 (PCM), panga I (EGM), jembe 1(EGM, PCM na EBuCA), reki 1 (EBuCA), mifagio 2 wa ndani (PCM) na wanje (EGM na EBuCA).

(x) Koti la maabara kwa wanafunziwa mchepuo wa **PCM**

2.3.Michango mbalimbali ya shule

| NA. | AINA YA MCHANGO | KIASI |
|---|---|---|
| .1 | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2. | Nembo | 5,000/= |
| 3. | Kitambulisho | 5,000/= |
| 4 | **Tahadhali** | **5,000/=** |
| | **JUMLA** | **80,000/=** |

Malipo haya yote yalipwe kwenye akaunt ya shule namba ya **akaunt NMB:5111100028 Jina la akaunti PUGE ELIMU YA KUJITEGEMEA**

**3. SHERIA NA KANUNI MUBIMU ZA SHULE**



CamScanner

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa sheria Na. IO ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Rais – TAMJSEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuata0;

3.1.Sheria na kanuni za shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
vii. Kutunza mali za shule;
viii. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari;
ix. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU**

I. Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yeyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.
II. Mwanafunzi awapo shuleni anatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye bweni ambalo halrupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu.
III. Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa mkuu wa shule kwa (msiba na ugonjwa).
IV. Mwanafunzi kamwe haruhusiwi kuja na nguo za kawaida (za nyumbani).

**3.2. Makosa yanayosababisha mwanafunzi kufukuzwa shule ni pamoja na:**

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo wa aina yeyote ile
iv. Kutoa lugha chafu kwa mwanafunzi mwenzake, walimu/walezi au jamii kwa ujumla
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kujaribu au kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika – Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote.
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya ya aina yeyote.
viii. Uvutaji wa sigara aina yeyote,
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsia moja/kuoa au kuolewa
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yeyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
xiv. Kudharau bendera ya Taifa
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiuwa, au kutishia kujiuwa kama kunywa sumu na
xvi. Uharbifu wa mali za Umma kwa makusudi

## 4. VIAMBATISHO NA FOMU MUHIMU

i. Fomu ya uchunguzi wa afya (Medical examination form) (Fomu Na.1) ambayo itajazwa na Mganga mkuu wa hospitali ya serikali.
ii. Fomu ya Maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/maktaba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai (Fomu Na.2).

Aje viambata na fomu hizo zikiwa zimekamilika.

# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

## PRIME MINISTER'S OFFICE

## REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

## FORM FOR MEDICAL EXAMINATION

**To be completed by a government Medical Officer** in **respect of all Form I and Form V entrants.**

STUD'ENT'SNAME: ••••••••••••••••••••••••••••••••••••••••••••••••••••••••••••••••••••••••

Please examine the student named above and comment on his/her health recording to the following items.

Kindly put a tick in out of either YES or NO whichever is applicable.

**Does the student have problem** in **connection with**

**A.** -**Sight?** **I.NO** ..- ---
1F YES .state 2.YES .B.
Hearing? !NO .
IF YES state 2.YES ..
C. TB? ..-.............................................................. 1.NO .
IF YES state......·..·.........2. YES..............
D. Blood Pressure? I.NO . - - - - ............
IF YES state 2."YES. - - ........... - - - - -
E. Any other health problem? I. NO ..
IF ms state 2.YES .
F. Syphilis and other veneral disease? \
IF YES state 2.YES .
No please, state! .

Name: Signature: .
Designation........................................ Date:................... Official Stamp

FOMU NA.2

**TAARIFA ZA MAZAZI/MLEZI NA AHADI YA MZAZI KUKUBALIANA NA MASHARTI YA MWANAE KUJIUNGA NA SHULE BIL**

1. Jina la mwanafunzi:
2. Tarehe ya kuzaliwa:
3, Amezaliwa katika wilaya: ..................................................................
4. Uraia..................
5. Mabali.anapoishi kwa sasa:
   (i) Wilaya: Tarafa.
   Kata: ............................................ Mtaa/Kijiji
6. Dini: ...........
7, Jina la Mzazi/Mlezi:
   (a) Anwani ya mz.azi/Mlezi: (Mabadiliko yawasilisbwe ofisini mara moja)
   (b) Simu ya (nyumbani/mkononi)...........................................
8. Unataarifiwa kuwa shule hii ni shule ya Serikali wala siyo ya DINI yoyote. Aidha inazingatia katiba ya nchi kuhusu uhuru wa kuabudu. Hivyo, kila siku ya Ijum.aa, Jumamosi na Jumapili wanafunzi huruhusiwa kwenda sehemu za ibada kulingana na Imani zao, Aidha, vimepangwa vipindi viwili vya dini katika ratiba za masomo kwa siku ya Ijumaa na kila siku jioni huwa na kipindi cha dini baada ya chakula kuanzia saa 1:00-130usiku Wanafunzi haruhusiwi kuanzisha ratiba yao ya kuabudu katikati ya vipiodi na .ratiba zingine za shule. Mzazi amshauri mtoto vizuri kuzingatia agizo hili bila kuleta sababu zozote.
9. Ahadi ya mwanafunzi:.........................................................................................

   Ninakubali/Sikubali kutii kikamilifu Kanuni, Sheria na Maagizo ya Shule yaliyotolewa hapo, kinyume cha hayo ni kufukuzwa shule na ndiyo mwongozo wangu mpaka kumaliza shule.
   Saini ya Mwanafunzi:
10. Ahadi ya mzazi/Mlezi: Mimi
   Nakubaliana/Sikubaliani na maagizo yaliyotolewa hapo juu. Naahidi mwanangu akienda tofauti afukuzwe shule.

**Jina la Mzazi/Mlezi:**.............................................. **Saini:**...................... **Tarehe:**...........

| PICHA NA.I | PICHA NA.2 | PICHA NA.3 | PICHA NA.4 |
|---|---|---|---|

Zibandikwe picha za wazazi/walezi watakaotambulika shuleni pamoja na namba zao za simu.

Mwanafunzi aje na picha mbili (2) (passport size) za kwake na picha nne (4) za walezi (passport size).

NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mtandao).

Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.

TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: •

- Mkuu wa shule: 0683797471/0679797471
- Makamu mkuu wa shule: 0783123777

5, Tafadhali soma kwa makini Maelezo/Maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI PUGE**

Sahihi ya Mkuu wa Shule ..................................................

Mhuri wa Mkuu wa Shule